

**HALMASHAURI YA WILAYA MASASI**  
(Barua zote zielekezwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

Simu: 2510031, 2510013.

Fax: 2510045.

E-mail: [ded.masasidc@gmail.com](mailto:ded.masasidc@gmail.com)



S.L.P. 60,  
Masasi,

Mtwara,  
Tanzania

Unapojibu tafadhali taja:

**Kumb. Na. MDC/S.20/31/68**

**Tarehe. 12/08/2020**

# TANGAZO

**YAH: NAFASI ZA KUHAMIA KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA MASASI  
KUTOKANA NA UTEKELEZAJI WA IKAMA NA BAJETI YA MISHAHARA YA  
MWAKA 2019/2020 KUHUSU KUWABADILISHA KADA WATUMISHI  
(RECATEGOLIZATION)**

Marejeo yanafanywa kupitia barua yenye kumb.**Na.BC.46/97/03 "TEMP"/01** ya tarehe 18Juni, 2019 iliyohusu utekelezaji wa zoezi la kuwabadilisha kada (**Recategolization**) watumishi kwa ikama ya mwaka 2019/2020.

Kufuatia barua hiyo, Serikali imeelekeza kuendelea na utekelezaji wa Ikama na Bajeti tajwa hapo juu, na kwa mamlaka iliyonayo Halmashauri chini ya kifungu Na. 6(1) (b) cha sheria ya Utumishi wa Umma Sura Na. 298, Halmashauri akiwa ndiye mwajiri anatakiwa kuendelea kuwabadilisha kada (**Recategorization**) watumishi waliotengewa nafasi katika Ikama na Bajeti ya mwaka wa Fedha 2019/2020.


Serikali pia imeelekeza kwamba, kwa madhumuni ya kuhakikisha utekelezaji wa zoezi hili unafanyika kwa wakati na ufanisi, Halmashauri ya Wilaya ya Masasi kwa kuzingatia masharti na maelekezo yote yaliyobainishwa kupitia waraka wa Katibu Mkuu (UTUMISHI) wenye Kumb. Na. C/AC.44/45/01/A/83 wa tarehe 1 Desemba, 2009 kuhusu utaratibu wa kuwabadilisha kazi (Recategorization) watumishi wa umma ambao wamejiendeleza katika Nyanja tofauti na zile walizokuwa wakifanyia kazi pamoja na waraka wa utumishi wa umma Na. 1 wa mwaka 2011 wenye Kumb.Na. CAC.44/45/01/A/121 wa tarehe 20Desemba, 2011 kuhusu utaratibu wa kuwabadilisha kazi (Recategorization)/kuwapandisha vyeo walimu wa shule za Serikali ambao wamejiendeleza kielimu.

Nawatangazia watumishi wa Serikali ambao wanasifa za kuomba kuhamia ili wabadilishwe kada baada ya Halmashauri kukosa watumishi wenye sifa kwa mujibu wa miundo ya utumishi katika kada zifuatazo;

1. Computer Technician II Nafasi 2
2. Supplies Officer II Nafasi 1
3. Accountant II Nafasi 5
4. ICT Officer II Nafasi 4
5. Community Development Officer II Nafasi 1
6. Social Welfare II Nafasi 1
7. Health Secretary-Nafasi 1
8. Clinical Officer II Nafasi 5
9. Legal Officer II Nafasi 1
10. Ward Executive Officer II Nafasi 1
11. Veterinary Officer II Nafasi 1

Kwa wale watakao fanikiwa kuhamia ubadilishaji vyeo huo utahusu Watumishi waliojipatia sifa za kielimu na taaluma kama ilivyoainishwa kwenye miundo ya kada zao pamoja na masharti yaliyoelekezwa kwenye Kanuni D.40 (1) (2) ya Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma, Toleo la Mwaka 2009 isipokuwa makundi ya watumishi wa kada za Mtendaji wa Kata ambao utaratibu wao wa kubadilishwa kada (Recategorization) ulielekezwa kwenye Waraka wa Katibu Mkuu (UTUMISHI) Na. CCA.271/431/01/H/67 wa tarehe 01 Agosti, 2019 aya ya 3 (a)(b) na (c).

Hivyo waombaji wote mtazingatia taratibu za uhamisho wa kawaida mkiwa katika kada zenu za sasa isipokuwa mnatakiwa kubainisha kwamba uhamisho huo unazingatia baruaa hii na uoneshe nafasi unayoitaka katika orodha hapo juu.



Changwa M Mkwazu

MKURUGENZI MTENDAJI (W)

MASASI